**HOTUBA YA WAZIRI WA MADINI, MHESHIMIWA ANTHONY PETER MAVUNDE (MB.) WAKATI WA KUFUNGA MAONESHO YA SITA YA TEKNOLOJIA YA MADINI TAREHE 30 SEPTEMBA, 2023.**

- Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman na Mgeni Rasmi wa shughuli hii ya leo.Mheshimiwa Martin Reuben Shigella - Mkuu wa Mkoa wa Geita;
- Waheshimiwa Mawaziri Wote Mliopo hapa;
- Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa jirani ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Simiyu;
- Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Geita;
- Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini-Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi (Mb);
- Kamati za Usalama;
- Waheshimiwa Manaibu Waziri;
- Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini;
- Makatibu Wakuu mliopo hapa;
- Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini;
- Naibu Makatibu Wakuu mliopo hapa;
- Mwenyekiti wa Tume ya Madini;
- Makatibu Tawala wa Mikoa wakiongozwa na Mohamed Jumanne Gombati - Katibu Tawala Mkoa wa Geita;
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;
- Waheshimiwa Wabunge,
- Wakurugenzi wa Halmashauri Mkoa wa Geita;
- Wenyeviti wa Halmashauri na Madiwani Wote Mliopo;
- Viongozi wote wa Serikali na Taasisi Mbalimbali;
- Viongozi wa Chama Cha Wachimbaji Wadogo wa Madini (FEMATA na

GEREMA);

- Wawakilishi toka Migodi na Makampuni ya Uchimbaji Madini;
- Wadhamini na wadau wote wa Maonesho;
- Viongozi wote wa Dini na Madhehebu mbalimbali;
- Washiriki wa Maonesho;
- Wanahabari, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania"**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki kikamilifu katika maonesho ya sita ya Teknolojia ya madini ambayo yatahitimishwa siku ya leo. Pia, tunakushukuru Mheshimiwa Mgeni Rasmi kwa kutenga muda wako pamoja na majukumu mengi uliyonayo na kuona umuhimu wa kuja kutufungia Maonesho haya yaliyobeba kauli mbiu isemayo **''Matumizi sahihi ya Teknolojia katika kuinua Wachimbaji Wadogo Kiuchumi na Kuhifadhi Mazingira"**. Aidha, kipekee nikushukuru wewe binafsi Mheshiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuongoza Wizara ya Madini. Mimi na viongozi wenzangu wa Wizara tunakuahidi kuwa tutafanyakazi kwa bidii, weledi na tutaendelea kupokea maelekezo na miongozo yako katika kusimamia na kuhahakikisha sekta ya madini inachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mheshimiwa Martin Reuben Shigella, Viongozi, Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi pamoja na Wananchi wa Mkoa wa Geita kwa kufanikisha maonesho haya. Napenda pia,

kuchukua fursa hii kuwapongeza wadau mbalimbali waliodhamini na kufanikisha maonesho haya wakiongozwa na Kampuni ya Geita Gold Mine Limited. Nawapongeza wote kwa kuendelea kuelimisha umma kuhusu fursa na huduma mbalimbali wanazotoa kwa jamii hasa kuendeleza na kuimarisha Sekta ya Madini. Mchango wao umekuwa na tija na mafanikio katika sekta yetu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** kipekee kabisa napenda pia kuchukua fursa hii kushukuru Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Halmashauri ya Mji wa Geita kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kuandaa na kufanikisha maonesho ya sita ya Teknolojia ya Madini ya mwaka huu. Ushirikiano wao umewezesha maonesho haya kufanyika kwa mafanikio makubwa sana. Hongereni sana.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Maonesho haya yamebeba Dhana ya kuwaelimisha wadau wa sekta ya madini kuhusu matumizi sahihi ya teknolojia katika kuwainua Wachimbaji wadogo na uhifadhi wa mazingira. Dhana hii inaenda sambamba na Sera ya Madini ya Mwaka 2009 pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM inayoielekeza Serikali kuwawezesha wachimbaji wadogo kujiajiri kupitia sekta hii kwa kuwatambua, kuwapatia mafunzo, teknolojia na maarifa ya kisasa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uchimbaji madini.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Katika maonesho haya dhana hiyo imetekelezwa kwa vitendo kupitia utoaji wa elimu na mafunzo kwa wadau walioshiriki katika maonesho ambapo fursa mbalimbali zilibainishwa kwa wananchi pamoja na uwezekano wa upatikanaji wa teknolojia na mitaji hasa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Aidha, katika maonesho haya elimu ya utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini imetolewa tangu maonesho haya yalipoanza tarehe 20 Septemba, 2023 hadi kufikia leo tarehe 30 Septemba, 2023. Nawashukuru sana wananchi na wadau wengine kwa kushiriki kwa wingi katika maonesho haya ambayo yamefana sana na niwaombe mjitokeze na kushiriki kwa wingi katika maonesho yajayo.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** maonesho haya tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018, yamekuwa na mchango mkubwa katika kutangaza fursa zilizopo katika sekta ya madini, kutoa

elimu na kuhamasisha matumizi sahihi ya Teknolojia za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini pamoja na kuwaunganisha wachimbaji wadogo na taasisi za fedha ili waweze kukopeshwa mitaji. Mathalani, jumla ya wachimbaji wadogo (Takwimu za uzalishaji na idadi ya wachimbaji wadogo walifaidika kwa kubadili njia za uchimbaji kwa kutumia teknolojia na mitambo ya kisasa) –takwimu ziwekwe.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Ni ukweli usiopingika kuwa Sekta ya Madini ni nguzo muhimu na ni chachu ya maendeleo duniani kote. Hivyo, ili madini yetu yaweze kubadilisha uchumi wa nchi na maendeleo ya wananchi, Wizara inaendelea kusimamia shughuli za sekta ya madini ili kuhakikisha kuwa zinafungamanishwa na sekta nyingine za kiuchumi. Mimi na Viongozi wenzangu wa Wizara tumejiwekea maono yenye kaulimbiu isemayo "Vision 2030 **Madini ni Maisha na Utajiri".** Kupitia kaulimbiu hii Wizara imelenga kufanya utafiti kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya *High Resolution Geophysical Survey* angalau kufikia asilimia 50 ya eneo la nchi nzima ifikapo mwaka 2030. Gharama za utafiti huo ni kubwa na kwa sasa Wizara inatafuta fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo na Serikali ili kuiwezesha taasisi ya GST kutekeleza jukumu hilo.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** ni imani yetu kwamba, baada ya kufanyika kwa utafiti huo tutafahamu tabia na aina mbalimbali za miamba nchini yenye viashiria vya uwepo wa madini mbalimbali. Kutokana na uwepo wa taarifa hizo za kijiolojia uwekezaji katika sekta ya madini utaongezeka kwani itakuwa rahisi taarifa hizo kutumika kufanya utafiti wa kina katika maeneo mbalimbali ya nchi na hivyo kuongeza fursa ya kuanzishwa kwa miradi ya uchimbaji madini hapa nchini.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**, mpango huu utawezesha kuongeza wigo wa kufungamisha Sekta ya madini na sekta nyingine za uzalishaji kama vile Sekta ya kilimo, Maji, Viwanda na Bisahara kupitia ugunduzi wa

maeneo yenye viashiria vya uwepo wa maji na madini mbolea kama vile phosphate, potash, Sulfur, chokaa (limestone), jasi (gypsum) na Nitrojeni na hivyo kufanya utafiti wa kina katika maeneo husika kwa ajili ya kugundua mashapo ya madini hayo kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea ya kutosha nchini.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, mpango huu utawezesha pia Serikali kuendesha programu za uchorongaji na utafiti wa kina katika maeneo yenye viashiria vya madini kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili kujua kwa uhakika mashapo ya madini yaliyopo katika maeneo yao. Kwa miaka muda mrefu wachimbaji wamekuwa wakitengewa na kuchimba madini katika maeneo ambayo taarifa za kijiolojia hazijulikani na hivyo kuendesha shughuli zao kwa kubahatisha. Uchimbaji wa aina hii umekuwa hauna tija kwao. Kwa kuwekeza na kufahamu taarifa za kijiolojia katika maeneo yao kutafanya wachimbaji wadogo waendeshe shughuli zao kwa uhakika na kuongeza mchango wao katika uchumi wa taifa. Mambo yote haya niliyoyaeleza ndiyo yanayobeba na kutafsi kaulimbiu ya "**Vision 2030 Madini ni Maisha na Utajiri**"

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Baada ya kusema maneno hayo mafupi kwa heshima kubwa nikuombe na kukukaribisha ili uweze kuongea na hadhara hii ya washiriki na wananchi waliopo mbele yako na hatimaye utufungie maonesho haya ya Sita ya Teknolojia ya Madini kwa Mwaka 2023.

**KARIBU SANA MHESHIMIWA MGENI RASMI.**